

MAELEZO YA MSINGI JUU YA MASHINDANO YA KIHISTORIA YA RIADHA BAGAMOYO

KARIBU NA JUMUIKA NASI KATIKA “BAGAMOYO RACE THROUGH HISTORY”

Yafuatayo ni maelezo ya msingi kuhusu tukio hili la kimichezo. Marekebisho yaweza kujitokeza kulingana na maoni ya wadau na vilevile maelekezo kutoka mamlaka mbalimbali husika.

(I) Mahali, Muda na tarehe: Mashindano haya ya riadha kwa jina “*Bagamoyo Race Through History*” yatafanyika mjini **Bagamoyo** yakipitia sehemu mbalimbali za kihistoria kama vile Magofu ya Kaole, Boma la Zamani la Wajerumani, Mnara wa Kale wa Kania, n.k. Mashindano yatafanyika tarehe 31/7/2010 kama ifuatavyo:

1. Saa 2 – 2 dk 15 (ASUBUHI) – Mgeni rasmi Kuwasili
2. Saa 2 dk 30 – Mbio za Kilometa 10 kuanza
3. Saa 3 dk 30 – Mbio za Kilometa 5 (Washiriki binafsi na timu za Mashirika, Kampuni, Mamlaka za serikali, Taasisi na balozi mbalimbali ambapo kila timu huwa na wachezaji wa-nne).
4. Saa 5 kamili – Utoaji zawadi kwa washindi.
5. Saa 1 USIKU – TAFRIJA MAALUM (Kutegemea na mwitikio wa wadau)



(II) Maelezo mengine muhimu

(a) Umbali na aina za mashindano kwa mwaka huu :

1. Kilometa 10 kwa washiriki binafsi
2. Kilometa 5 kwa “**Business Class Team Competition**” ambapo timu za Mashirika, Kampuni, Mamlaka za serikali, Jumuiya, Taasisi na Balozi mbalimbali au hata timu za Marafiki zitashindana. Kila timu itakuwa na wachezaji wa-nne (4) ambao muda wa kila mchezaji utajumlishwa na muda wachezaji wa timu yake hatimaye mshindi kupatikana.
3. Kilometa 5 kwa washiriki binafsi

(b) Ada za mashindano (*Malipo kwa njia ya Hundi yalipwe kwa: Shemweta Invest AB, P. O Box 106240, Dar Es Salaam*)

1. Washiriki binafsi wazawa TZS. 500/=
2. Washiriki binafsi wageni TZS. 5 000/=
3. Timu shiriki (*Business Class teams*) TZS. 50 000/=
4. Kiingilio cha TAFRIJA MAALUMU TZS. 50 000/=

Kumbuka: Ada ya ushiriki ikishalipwa haitarudishwa isipokuwa tu pale waraka maalumu wa uthibitisho (kutoka kwa Daktari au Jeshi la Polisi) wa sababu za kujitoka, kutolewa kabla ya mashindano kuanza.

(c) Zawadi (zitatangazwa baadaye) ni kama ifuatavyo :

1. Washindi 3 wa mwanzo kwa wanaume na wanawake – Kilometa 10
2. Washindi 3 wa mwanzo kwa wanaume na wanawake – Kilometa 5
3. Washindi 3 wa mwanzo kwa wanaume na wanawake kwa ndugu zetu wenye ulemavu – Kilometa 5
4. Washindi 3 wa mwanzo katika “*Business Class Team Competitions*” (Vyeti)



*Vyeti kwa washiriki wengine vyaweza kuagizwa kwa gharama ya TZS 2 000/= kwa kila cheti ambapo mhusika atakichukua cheti chake kwenye ofisi za **Shemweta Invest AB** siku chache baada ya mashindano. Iwapo mhusika atapenda basi cheti hicho chaweza kuwekwa kwenye fremu maalum kwa gharama ya nyongeza..*

TUNAWATAKIA NYOTE USHIRIKI MWEMA WA MASHINDANO HAYA YA RIADHA BAGAMOYO!

INVITATION FOR A HISTORIC RUNNING EVENT IN BAGAMOYO

WELCOME TO BAGAMOYO RACE THROUGH HISTORY

The following are preliminary information regarding this road race event. Slightly adjustments may be made due to several inputs and directions from other stakeholders and authorities respectively.

(I) Venue, date and time: *Bagamoyo Race Through History* will be held in **Bagamoyo town** passing through several historical sites such as Kaole Ruins, Old German Boma, Old Church tower, etc. - on July 31, 2010 at

1. 0800 - 0815 hrs - Guest of Honour arrives
2. 0830 hrs - starts for 10 km race
3. 0930 hrs - starts for 5 km race (Business Class Team Competition & individuals)
4. 1100 hrs - Award ceremony
5. 1900 hrs – BAGAMOYO SPORTING BANQUET (Depending on stakeholders)

(II) Other essential information

(a) Race categories for this year :

1. 10 km for individuals
2. 5 km **Business Class Team Competition** for private and public companies, governmental and non-governmental organizations, foreign missions and embassies as well as clubs-mates and/or trainings partners (4 runners per team)
3. 5 km for individuals



(b) Entry fees are as following (*Cheque made payable to Shemweta Invest AB, P. O Box 106240, Dar Es Salaam*)

1. Individual native participant TZS. 500/=
2. Individual foreign participant TZS. 5 000/=
3. Business Class teams TZS. 50 000/=
4. Admission ticket to BAGAMOYO SPORTING BANQUET TZS. 50 000/=

Note: Entry fees are non-refundable unless a certified document from a Doctor or Police Force is provided prior to start.

(c) Prizes (to be announced later) are as following :

1. 3 top positions for men and women categories 10 km
2. 3 top positions for men and women categories 5 km
3. 3 top positions for men & women wheelchair participants in 5 km.
4. 3 top positions for Business Class Team Competitions (Certificates)



*Official certificates for the rest of participants can be ordered at the cost of TZS 2 000/= each and shall be collected at **Shemweta Invest AB** offices few days or so after the race. If agreed, the certificate can be placed (secured) in a special made frame at an extra cost.*

WE WISH YOU A PLEASANT PARTICIPATION IN BAGAMOYO AND GOODLUCK!